

**Hotuba ya Mgeni Rasmi Mhe Selemani Jafo (Mb) Naibu Waziri wa
Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwenye Mkutano wa Mikoa
Inayotekeleza Mradi wa RBF, Tarehe 24/06/2017 Katika Ukumbi
wa Rock City Mall Mkoani wa Mwanza.**

Ndg. Naibu Katibu Mkuu (A) –OR-TAMISEMI

Ndg. Mkurugenzi wa Idara ya Afya Ustawi wa Jamii na Lishe –OR-
TAMISEMI

Mkuu wa Wilaya ya Ilemela Mhe. Masale

Makatibu Tawala wa Mikoa ya Shinyanga Mwanza Pwani Simiyu Tabora
Geita, Kagera na Kigoma

Mstahiki Meya wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza

Mwakilishi wa Wizara ya Fedha na Mipango

Wawakilishi wa Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na
Waatoto

Wadau wetu wa Benki ya Dunia

Wakurugenzi OR-TAMISEMI na MoHCDGCE

Wahe. Ma-Mayor/Wenyeviti wa Halmashauri

Wakurugenzi wa Halmashauri

Waganga Wakuu wa Mikoa

Waratibu wa RBF wa Mikoa

Waganga Wakuu wa Halmashauri

Waratibu wa RBF wa Halmashauri

Wageni waalikwa Mabibi na Mabwana

“Asalaam Aleikum”

“Bwana yesu Asifiwe”

Kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kumshukuru mwenyezi Mungu kwa kutujaalia Afya njema na kutuwezesha kukutana siku ya leo kwa ajili ya mkutano huu muhimu. Pili napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa kuweza kupata nafasi hii ya kuwa mgeni rasmi katika mkutano huu muhimu.

Tatu napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwanza kwa waandaaji wa mkutano kwa maandalizi mazuri, pili kwa washiriki wote kwa kuitikia wito wa kuhudhuria mkutano huu, hongereni sana.

Ngugu washiriki,

Leo tumekusanyika hapa viongozi na watendaji kutoka ngazi ya taifa, Mikoa na Halmashauri zetu katika mkutano huu muhimu wa malipo kwa ufanisi (RBF) unaotekelezwa chini ya program ya uimarishaji wa mifumo ya huduma za Afya ya Msingi kwa matokeo (Primary health care system strengthening for results).

Lengo kuu la mkutano huu ni kujadili mafanikio mbalimbali yaliyopatikana katika utekelezaji wa mradi wa RBF, lakini pia kubaini changamoto mbalimbali zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa mradi, kwa lengo la kuweza kutafuta mbinu za kukabiliana na changamoto hizo, ili tuweze kuboresha na kutekeleza mradi huu kwa ufanisi zaidi. Aidha mkutano huu pia utatoa nafasi ya washiriki kujifunza na kubadilishana uzoefu baina ya Halmashauri zinazofanya vizuri na zile ambazo bado zinasuasua katika utekelezaji wa mradi wa RBF.

Ndugu washiriki,

OR – TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Afya maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto kwa pamoja tunatekeleza program ya uimarishaji

wa huduma za Afya ya uimarishaji wa mifumo ya huduma za Afya ya Msingi kwa matokeo (Primary health care system strengthening for results). Mradi huu wa (PHSSR) unatekelezwa kwa muda wa miaka 5 katika maeneo makuu matatu kama ifuatavyo: -

- i. Kuchangia katika mfuko wa pamoj wa Afya (Basket Fund) kwa kipindi chote cha miaka 5 (mitano) ya utekelezaji wa mradi, ambapo fedha katika eneo hili zitatolewa kwa kufuata taratibu za uendeshaji wa shughuli za kawaida za mfujo wa pamoja wa Afya yaani Basket Fund.
- ii. Eneo la program kwa matokeo (Program for Results), ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa shughuli za tekeleza kwa matokeo makuwa sasa (BRN).
- iii. Mradi wa malipo kwa ufanisi (Result based financing-**RBF**). Mradi huu utatekelezwa nchi nzima, na mikoa itakuwa inaingia katika utekelezaji wa awamu. Aidha fedha katika eneo hili zitakuwa zinatolewa kwa kuzingatia matokeo yatakayokuwa yanapatikana baada ya kufikia viashiria.

Ndugu washiriki,

Naomba sasa nichukue fursa hii kujikita zaidi katika mradi wa malipo kwa ufanisi (RBF) ambo ndio lengo kuu la mkutano huu.

Ndugu washiriki,

Naambiwa kuwa mradi wa malipo kwa ufanisi ulianza kutekelezwa hapa nchini mwaka 2015, katika Halmshauri ya Wilaya ya Kishapu Mkoani Shinyanga, ambao ulianza kama sehemu ya majaribio. Aidha baada ya kuona mafanikio makubwa yaliyopatikana Wilayani Kishapu, baadae mwaka 2016, mradi huu ulienezwa katika Halmashauri zote za Mkoa wa Shinyanga, na baadae katika Halmashauri zote za Mikoa ya Mwanza, Pwani, Tabora na Simiyu. Aidha hivi karibuni mradi huu utaenezwa katika Mikoa ya Kigoma, Geita pamoja na Kagera, na hivyo kufanya mradi huu kutekelezwa katika Mikoa 8 (nane) ya Shinyanga, Mwanza, Pwani, Simiyu,

Tabora, Geita, Kigoma na Kagera. Aidha katika utaratibu huu Mkoa wa Mara utatumika kama Mkoa linganifu (Control Region).

Ndugu washiriki,

Suala la kuuweka Mkoa wa Mara kuwa ni Mkoa linganifu maana yake ni kwamba, baada ya mradi kukamilika, Mikoa iliyotekeleza mradi wa malipo kwa ufanisi (RBF) italiganishwa na Mkoa wa Mara katika viashiria vyote vilivyokuwa vinafuatiliwa wakati wa utekelezaji wa mradi. Changamoto itakuwa ni pale itapojitokeza kuwa Mikoa iliyotekeleza mradi wa RBF kufanya vibaya kuliko Mkoa wa Mara (Mkoa linganifu).

Ndugu washiriki,

Utekelezaji wa mradi wa malipo kwa ufanisi katika Mikoa iliyoaniza kutekeleza mradi, umekabiliana na changamoto kadhaa, baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na:-

- (i) Mwingiliano wa kimajukumu, katika utekelezaji wa mradi kati ya Ofisi ya Rais TAMISEMI pamoja na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto kwa mfano: Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto ikiwa na jukumu la kutunga sera, miongozo na kusimamia ubora wa huduma, ndio imeonekana kuwa mtekelezaji mkuu wa mradi huu wa malipo kwa ufanisi.
- (ii) Kasi ndogo ya utekelezaji wa mradi, kwani utaratibu wa mikoa ya majaribio (Pilot Regions) kuchukua muda mrefu, hivyo kuchelewesha mradi kuenea kwenye Mikoa mingine. Hali hii imesababisha matokeo ya mradi huu kutoonekana nchi nzima jambo lililosababisha utoaji wa huduma za afya kuendelea kuwa

chini kwa mfano kuendelea kuongezeka kwa vifo vya akina mama wajawazito hapa nchini, ambavyo vingeweza kupunguzwa kwa kutumia fursa ya mradi huu.

- (iii) Matumizi madogo ya fedha zilizotengewa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu katika ngazi za mikoa na Halmashauri, jambo linalosababisha malengo ya mradi kutokufikiwa kama ilivyopangwa. Hii inamaana kuwa, ikiwa utumiaji wa fedha bado utaendelea kwa kusuasua, fedha nyingi zitabaki pale itakapofika mwisho wa mradi ambapo serikali italazimika kuzirudisha fedha hizo Benki ya Dunia, wakati wananchi wetu bado watakuwa na matatizo mengi ya kiafya.
- (iv) Usimamizi hafifu wa utekelezaji wa mradi hususani katika ngazi za mikoa na Halmashauri, hali inayosababisha matokeo yaliyotarajiwa kushindwa kuonekana kwa wakati.
- (v) Watumishi kufanya kazi kwa mazoea, bila kuzingatia matokeo katika utendaji kazi wao.
- (vi) Fedha zinazotumwa katika Halmashauri kuto kupelekwa moja kwa moja katika akaunti za vituo vya kutolea huduma za Afya, kama taratibu za mradi zinavyotaka jambo linalosababisha fedha hizo kutofika kwa wakati na hivyo kuchelewesha utekelezaji wake.

Ndugu washiriki,

Ni matumaini yangu kuwa kikao hiki kitachambua kwa kina changamoto zote nilizozibainisha hapo juu, pamoja na changamoto nyingine zitakazojitokeza wakati wa mjadala na kutafuta majawabu sahihi juu ya namna bora ya kutekeleza mradi huu ili kuleta matokeo yaliyotarajiwa.

Ndugu washiriki

Mradi wa malipo kwa ufanisi (RBF) ni fursa muhimu katika kuboresha huduma za Afya hapa nchini, aidha uzoefu kutoka nchi nyingine

zilizotekeleza mradi huu vizuri mfano nchi ya Rwanda, unaonesha kuwa, kuna mabadiliko makubwa ya kiutendaji kazi pamoja na ubora wa huduma za Afya nchini humo. Aidha utoaji wa huduma za Afya umeboreshwa kwa kiasi kikubwa kwenye Halmashauri zilizotekeleza na kusimamia vyema mradi huu, kwa mfano katika Halmashauri za Mkoa wa Shinyanga.

Ndugu washiriki,

Kutokana na sababu hizo na umuhimu wa mradi huu katika kuboresha huduma za Afya hapa nchini, napenda kutoa maelekezo yafuatayo ambayo pia ningependa nipate mrejesho katika utekelezaji wake: -

- (1) Kuwe na mgawanyo mzuri wa majukumu ya utekelezaji wa mradi huu pamoja na shughuli nyingine za Afya kati ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto pamoja na OR – TAMISEMI. Hii namaanisha kuwa kila taasisi itekeleze shughuli zake kwa mujibu wa sera ya ugatuuji wa madaraka kwenye ngazi za chini pamoja na kuzingatia mipaka ya kimadaraka baina ya Wizara hizi mbili. Aidha nasisitiza kuwa kila Wizara itekeleze wajibu na majukumu yake kama yalivyobainishwa kwenye Mwongozo wa RBF, na upimaji ufanyike kwa kuzingatia matokeo ya utekelezaji.
- (2) Kasi ya utekelezaji wa mradi huu iongezeke, aidha tujikite zaidi kutekeleza mradi huu kwa nchi nzima badala ya kuendelea na maeneo ya majaribio ili matokeo ya mradi yaweze kuonekana kwa nchi nzima badala ya kuonekana kwenye maeneo machache kama ilivyo sasa.
- (3) Ni vyema ikapangwa mikakati thabiti, ya kuongeza kasi ya utumiaji wa fedha za mradi huu. Aidha msisite kuwachukulia hatua watumishi waliopo chini yenu, ambao wataonekana kuzembea na kusababisha fedha za mradi huu zisitumike kama ilivyopangwa. Hii ikiwa ni pamoja na kuwachukulia hatua wagaga wakuu wa

- Mikoa, Waganga wakuu wa Halmashauri, Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri pamoja na waganga wafawidhi wa vituo vya kutolea huduma za Afya ambao wataonekana kuzembea na kusababisha vituo vyao kufanya vibaya na hivyo kuchangia katika matumizi madogo ya fedha zilizotengwa.
- (4) Watendaji na viongozi wote waliopo katika ngazi za Taifa, Mikoa, Halmashauri, Wafanye ufuatiliaji wa karibu wa mradi huu, ili kuhakikisha kuwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya mradi zinatumiwa vizuri, na tena kwa wakati, ili kuweza kuleta matokeo yaliyotarajiwa.
 - (5) Ofisi ya Rais TAMISEMI (Idara ya Afya) ikamilishe kwa haraka uandaaji wa mikataba ya utendaji kazi wa taasisi zilizopo chini yake, mikataba hiyo ianze kufanya kazi ya kuzipima taasisi husika, ili watumishi waweze kufanya kazi kwa kuzingatia matokeo yaliyotarajiwa, badala ya kuendelea kufanya kazi kwa mazoea kama ilivyo sasa. Aidha mrejesho wa matokeo ya upimaji wa utendaji kazi wa taasisi husika ni lazima ufanyike katika ngazi zote na hatua stahiki zichukuliwe kwa taasisi zitakazofanya vibaya ikiwa ni pamoja na kuwavua madaraka wakuu wa taasisi hizo.
 - (6) Na mwisho, ni vyema ofisi ya Rais TAMISEMI ikae na Wizara ya Fedha na Mipango ili kuhakikisha upelekaji wa fedha za RBF kwenye Mikoa na Halmashauri husika linazingatia mkataba uliosaniniwa kati ya Serikali na Benki ya Dunia. Aidha haitavumilika ikiwa fedha za RBF kwa ajili ya vituo vya kutolea huduma za Afya zikaendelea kupelekwa kwenye akaunti za Halmashauri, badala ya kupelekwa moja kwa moja kwenye akaunti za vituo husika. Aidha kama kuna changamoto yoyote inayosababisha kutokutekelezwa kwa suala hili, ni vyema ngazi za juu za Wizara hizi tatu zikatambua na kuchukua hatua stahiki ili kurekebisha hali hii.

Ndugu washiriki,

Narudia tena kwa kusema kuwa nawashukuru wandaaji wa Mkutano huu kwa kunialika kujumuika pamoja nanyi leo hii, aidha nashukuru pia kwa usikivu wenu na kuendelea kutekeleza mradi huu, pamoja na changamoto zilizopo. Natoa wito kwa Mamlaka zinazohusika katia ngazi zote, kusimamia mradi huu kikamilifu ili kuhakikisha kuwa matokeo yaliyotarajiwa yaweze kufikiwa na hatimaye kuweza kuboresha utoaji wa huduma za Afya hapa nchini.

``Baada ya kusema hayo, napenda kutamka Rasmi kuwa mkutano wa malipo (RBF) unaofanyika hapa katika ukumbi wa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza nimeufungua rasmi''.

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA

NA MUNGU AWABARIKI

**RATIBA YA MKUTANO WA MRADI WA MALIPO KWA UFANISI
(RBF), CHA TAREHE 24/06/2017, KATIKA UKUMBI WA MKUU
WA MKOA WA MWANZA.**

MUDA	MADA/TUKIO	MHUSIKA
2:00 - 2:30	Wageni waalikwa kuingia ukumbini na kujiandikisha	Washiriki
3:00	Mgeni rasmi, Naibu Waziri wa Nchi OR – TAMISEMI Mhe. Selemani Jafo kuingia ukumbini	NW (N)-OR- TAMISEMI Mhe. Selemani Jafo
3:00 - 3:10	Utambulisho	DHS/RBFCo (OR-TAMISEMI)
3:10 - 3:20	Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mwanza kutoa salaam za mkoa kwa washiriki	Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mwanza
3:20 - 3:30	Mkurugenzi – OR TAMISEMI (AUL) kueleza malengo ya mkutano, kisha kumkaribisha NKM(A)	DHS (A) OR-TAMISEMI
3:30 - 3:40	NKM (A) kuongea machache na kumkaribisha Mgeni Rasmi	NKM (A) Dkt. Zainabu Chaula
3:40 - 4:00	Mgeni Rasmi NW (N) OR-TAMISEMI Mhe. Selemani Jafo kuhutubia washiriki wa Mkutano	NW (N) OR- TAMISEMI Mhe. Selemani Jafo
4:00 - 4:05	Neno la shukurani	Mayor Nyamagana
4:05 - 4:30	Picha ya pamoja – Chai	MC

4:30 - 4:45	Mada ya kwanza: Dhana ya mradi wa malipo kwa ufanisi katika kuboresha huduma za Afya nchini	DHS/RBFCo(OR – TAMISEMI)
4:45 - 4:55	Majadiliano	Mwenyekiti
4:55 - 5:15	Mada ya pili: utekelezaji wa mradi wa malipo kwa ufanisi nchini	RBFco-(MOHCDGEC)
5:15 - 5:30	Majadiliano	Mwenyekiti
5:30 - 6:00	Mada ya tatu: Taarifa ya mafunzo ya RBF nchini Rwanda – Kigali	Dkt. Zainabu Chaula (NKM-A)/Dkt. Anna Nswilla
6:00 - 6:20	Majadiliano	Mwenyekiti
6:20 - 7:05	Mifano ya kuigwa <ol style="list-style-type: none"> 1. RMO Shinyanga 2. DMO Msalala 3. DMO Shinyanga DC 	RMO Shinyanga DMO Msalala DMO shy DC
7:05 - 7:20	Majadiliano	Mwenyekiti
7:20 - 8:20	CHAKULA CHA MCHANA	WOTE
8:20 - 9:20	Maazimio ya mkutano	M/kiti-Kamati ya Maazimio
9:20 - 10:00	Kufunga kikao	NKM (A) – OR - TAMISEMI